# Vitendo

Sasa umejifunza mambo mengi mapya kuhusu takataka, athari zake katika dunia na vipi kudhibiti takataka ili kupunguza madhara yake. Sasa ni wakati muafaka wa kubadilishana elimu. Njia rahisi na ya kufurahisha ni kufundisha watu walio wadogo zaidi kuliko wewe.

Kama unafanyakazi na watoto wadogo, shirikisha viwanja vya skuli au mazingira ya karibu na kufanya takataka ni kitu cha kufurahisha. Angalia shughuli zifuatazo:

## KITENDO 1: Uchunguzi wa takataka

**a) Ni aina gani za takataka tunazozalisha majumbani mwetu?. (orodhesha)**
**b) Tunazifanya nini takataka hizo? (jadili kutumia maarifa ya nyumbani )**
**c) Kuna matatizo gani?**
**d) Ni kiasi gani cha takataka unazozalisha? (Angalia ukaguzi wa takataka katika 'Kupata burudani')**

## KITENDO 2: Uelewa mzunguko wa maisha ya kitu ya kila siku

**a) Vifaa gani vimetumika kutengenezea vitu vya darasani: (i) madirisha, ubao, deski, ukuta, nguo, (orodhesha)?**
**b) Vifaa hivi vinatoka wapi?(jadili)**
**c) Itatokea nini kwa vitu hivi iwapo vitatupwa?**

## KITENDO 3: Muhoji mwanajamii


**a) Unakumbuka kijiji kilivyokuwa kabla ya kuingizwa hizi takataka nyingi?**
**b) Lini plastiki ulitumika katika kijiji chako kwa mara ya kwanza?**
**c) Kitu gani kinakukera katika kijiji chako kuhusu takataka za plastiki?**
**d) Nini chanzo kikuu cha takataka za plastiki katika kijiji chako?**
**e) Unapata hisia gani unapomuona mtu anachoma plastiki katika kijiji?**

**(Andika jawabu za usaili na jadili matokeo katika kikundi).**

## KITENDO 4: Dhana ya uchafuzi wa mazingira

**Ni aina gani ya uchafunzi wa mazingira unayoiona katika picha hizo hapo chini? Eleza unachoweza kukiona.**





(© ReCoMaP, Pedagogical Guide)

## KITENDO 5: Wakati wa chemsha bongo

**Oanisha maneno na maelezo yalo sahihi.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ....Takataka | ....malighafi | ....hifadhi | ....bidhaa |
| ....kusarifika | ....Mbolea | .....shimo-taka | ....sumu |
| ....vifurushi | ....madini | | |

A. Vifaa vya kimaumbile vilivyo muhimu kwa maisha.
B. Sehemu maalum zilizotengenezwa kwa utupaji wa taka taka kidogo.
C. Imetengenezwa kwa mali ghafi au vifaa vilivyosarifiwa tena watu wananunua kila siku.
D. Haidhuru inahifadhi bidhaa kabla ya kununuliwa, baadhi ya bidhaa hazina haja ya hifadhi hizo. Angalia bidhaa zenye upungufu huu.
E. Hiki kinaweza kukusanywa katika jamii yako na kutengezwa kitu kipya.
F. Njia ya maumbile ya usafirishaji mabaki ya chakula na vitu vinavyooza.
G. Kila kinachoweza kuwadhuru watu au mazingira ikiwa hakitotupwa vizuri kinaitwa hivi.
H. Tumia kwa busara epuka taka taka.
I. Metali inayotokana na mawe katika ardhi.
J. Mabaki ya chakula , karatasi na vitu vyengine unavyovitupa.